JARIDA MTANDAO LA ROBO YA PILI 2023/2024

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

www.ubungomc.go.tz/Kitengo cha Mawasiliano Serikalini/Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo




Elias Runeye Ntiruhungwa
Mkurugenzi Manispaa ya Ubungo

HALIUZWI

# TAHARIRI

**JARIDA LA ROBO YA PILI 2023/2024**

**TAARIFA YA MAFANIKIO YA MIAKA MITATU YA RAIS WA AWAMU YA SITA**

Manispaa ya Ubungo inasema asante kwa uongozi wa Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake Manispaa ya Ubungo imefanikiwa kupokea kiasi cha shilingi Bilioni 52.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kati ya hizo, Bilioni 27.4 ni fedha kutoka Serikali kuu, na Bilioni 25.3 ni fedha za mapato ya ndani ambazo zimeboresha miundominu ya Elimu, Afya, Masoko na Sekta mbalimbali.

Maendeleo ya wanaubungo yanaendelea kupiga hatua katika upande wa elimu ambapo Sekta ya elimu msingi jumla ya Bilioni 8.3 zimetumika katika ujenzi wa Shule mpya 5, madarasa 204, nyumba za walimu 4, matundu ya vyoo 192, ununuzi wa madawati 995, ukarabati wa madarasa 104.

Kwa upande wa Sekta ya Elimu Sekondari Manispaa imefanikiwa kujenga Shule maalumu ya wasichana alikadhalika na Shule 6 mpya za Kata, madarasa 247, nyumba za walimu 9, mabweni 9, matundu vya vyoo 123, majengo ya utawala 4, ununuzi wa viti na meza 2640, upatikanaji wa vifaa vya maabara na madarasa ya mafunzo ya TEHAMA kwa gharama ya Shilingi Bilioni 14.6 na wanafunzi wanaendelea kupata elimu katika mazingira bora.

Aidha, Kwa upande wa Idara ya afya Manispaa ya Ubungo imetumia Bilioni 7.4 kuboresha miundombinu ya afya ikiwemo kujenga Hospitali ya Wilaya, Vituo vya afya na Zahanati.

Sambamba na hayo Manispaa ya Ubungo imefanikiwa kufanya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ambapo jumla ya shilingi Bilioni 2.7 zimetolewa kwenye jumla ya vikundi 331 vya wajasiriamali vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Katika utekelezaji wa mpango wa kunusuru Kaya Masikini TASAF kiasi cha shilingi Bilioni 1.9 kimetolewa kwenye kaya za walengwa 2838 kwa ajili ya kuwakwamua kwenye umaskini uliokithiri.

**Tembelea Tovuti ya Ubungo Manispaa**
**www.ubungomc.go.tz**



## UBUNGO TUMEWASIKIA, TUMEWAFIKIA MIAKA MITATU YA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN TUMEFANIKISHA

Na Mwandishi wetu

Kwa kipindi cha miaka mitatu Manispaa ya Ubungo imepokea shilingi bilioni 52.7 kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kati ya hizo, Bilioni 27.4 ni fedha kutoka serikali kuu, na Bilioni 25.3 ni fedha za mapato ya ndani.

SEKTA YA AFYA
Bilioni 7.4 zimetumika kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya afya ikiwemo kujenga Hospitali ya Wilaya, Vituo vya afya na Zahanati.

ELIMU MSINGI
Bilioni 8.3 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya 5, madarasa 204, nyumba za walimu 4, matundu ya vyoo 192, ununuzi wa madawati 995, ukarabati wa madarasa 104.

ELIMU SEKONDARI
Bilioni 14.6 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa Shule maalumu ya wasichana ya Mkoa, Shule 6 mpya za Kata, madarasa 247, nyumba za walimu 9, mabweni 9, matundu vya vyoo 123, majengo ya utawala 4, ununuzi wa viti na meza 2640.

UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU
Bilioni 6.3 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala, ununuzi wa magari mawili, ukarabati wa Ofisi za Kata, ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi, upandishaji madaraja watumishi 2,392 na kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 1,761

HIFADHI YA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU
Bilioni 4.9 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa magari mawili ya kubeba taka, ukusanyaji wa taka ngumu, kusafisha mifereji ya maji pamoja na kusafisha mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa Km 150

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI
Bilioni 2.7 zimetumika kwa ajili ya vikundi 331 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu vimepatiwa mikopo.

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI - TASAF
Bilioni 1.9 zimetumika kwa ajili ya kaya za walengwa 2838 zimesaidiwa kukwamuliwa kwenye umasikini uliokithiri na kuongezewa kipato.

SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI
Milioni 428 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa Machinjio ya kuku Manzese, ujenzi wa Miundombinu Nane nane, kumiliki ekari 28 katika eneo la Kibesa kwa ajili ya shamba darasa.

BIASHARA NA UWEKEZAJI
Bilioni 3 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi cha Mlonganzila, ujenzi wa jengo la Mama Lishe, kumiliki kiwanda cha matofali, ujenzi wa miundombinu katika kituo cha mabasi cha Magufuli pamoja na ujenzi wa mabanda matatu ya wajasiriamali.

MIPANGO MIJI
Bilioni 1.3 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa kifaa cha kupimia ardhi (RTK), Ulipaji wa fidia kwa ajili ya utwaaji wa ardhi pamoja na uwekaji wa anwani za makazi



# SOKO LA KUKU MANZESE LABORESHWA

Na Mwandishi wetu

Manispaa ya Ubungo imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 1.3 kutoka kwenye mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa uboreshaji wa soko la Manzese maarufu soko la kuku.

Katika uboreshaji huo Manispaa ya Ubungo imepanga kujenga fremu za kisasa kwenye ghorofa ya sakafu tatu ambapo jumla ya fremu 39 zitajengwa na hadi sasa ujenzi upo asilimia 20 na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2024.

Akielezea ujenzi huo Ndg. Geofrey Mbwama Afisa Mfawidhi sehemu ya biashara na masoko wa Manispaa hiyo amesema Manispaa imedhamiria kujenga fremu za kisasa kwa wafanyabiashara wa soko hilo hususani wauza kuku ili kuwawezesha kufanya biashara zao kwenye maeneo rafiki yatakayovutia wateja wao na hivyo kuweza kukuza vipato vyao.

Mbwama ametoa rai kwa wafanyabiashara hao kuanza kufanya biashara zao kisasa hususani wafanyabiashara wa kuku ambapo miundombinu itakayokuwepo itawalazimu kutunza kuku kwenye majokofu mara baada ya kuchinja.

Aidha, Mbwama ameeleza kuwa uboreshaji wa soko unaenda sambamba na sheria ya upangaji miji kwa kuweka miundombinu ya kisasa ukizingatia Manzese ni "smart area" na pia ni katikati ya Mji.

Sambamba na hayo Mbwama ameeleza kuwa uboreshaji wa soko hilo pia ni moja ya mkakati wa Manispaa wa kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani ili kuiwezesha Manispaa hiyo kukusanya Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ya sekta za elimu, afya, uboreshaji wa masoko na miundombinu mbalimbali.

Kwa upande wake Mualami Muya mfanyabiashara wa soko hilo akimshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na uongozi wa Manispaa ya Ubungo kwa ujumla amesema uboreshaji wa soko hilo utasaidia wafanyabiashara wa soko hilo hususani wauza kuku kuwa na eneo salama la kufanya biashara zao tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

..............Inaendelea ukurasa wa 03



*Ujenzi wa vizimba vya wajasiriamali soko la kuku Manzese vikiwa vinaendelea kujengwa*

"Tunamshukuru sana Rais wetu na viongozi wetu wa Manispaa ya Ubungo kwa uboreshaji wa soko hilo na tunaahidi kuitunza miundombinu yake sambamba na utoaji wa ushuru wa soko kwa maslahi ya Manispaa yetu" alisema Mualami.

Mualami ameeleza kuwa ujenzi wa fremu zenye miundombinu ya kisasa kwa ajili ya biashara ya kuku sio tu utaboresha mazingira ya biashara lakini pia utaondoa hasara kwa wafanyabiashara pale ambapo kuku watahitajika kuhifadhiwa kwenye majokofu kwani hali ya sasa inawalazima kulipia kiasi cha Fedha ili kuhifadhi kuku wao na wakati mwengine kuku hao hupotea.

"Kuna muda mfanyabiashara anapata kuku kutoka Mikoani hadi wakifika mjini kuku hao wanachoka sana na ndipo itamlazimu muuzaji kuchinja kuku hao na kuwahifadhi kwenye majokofu ambayo kwa sasa tunalipia na bado mara zingine muuzaji anaweza kupoteza kuku hao kwenye majokofu hayo kiukweli tunafarijika sana na uboreshaji huu ambao utapunguza au kuondoa tatizo hili" Alisema Mualami.

Soko la Manzese Lina jumla ya wafanyabiashara 496 ambapo kati ya hao wafanyabiashara wanaouza kuku ni zaidi ya 100 huku wanaobaki wanajishughulisha na biashara za mama lishe na biashara mchanganyiko.

Pia soko la Manzese ni miungoni mwa masoko 13 ya Manispaa ya Ubungo ambalo pia ni miongoni mwa masoko manne yanayoboreshwa na Manispaa hiyo kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 likiwemo soko la Mabibo, soko la SIMU 2000 na soko la Mbezi.



# HITIMISHO LA ZOEZI LA ARDHI CLINIK UBUNGO, HATI 1,692 ZATOLEWA.

Na Mwandishi wetu

Ikiwa ni siku ya mwisho ya zoezi la ardhi Clinic katika Wilaya ya Ubungo lililofanyika katika viwanja vya Kimara Stopover kwa siku 28 kwa awamu ya kwanza ambapo jumla ya hati 1,692 zimetolewa sawa na asilimia 89.2 ya lengo kwa awamu ya kwanza iliyolenga kutoa hati 1,898.

Akifunga zoezi hilo Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Hashim Komba alisema kuwa, katika kuhakikisha utatuzi wa swala la urasimishaji kwa wananchi wa Ubungo linafanyika na kuindoa sintofahamu kwa wananchi ili kila mwananchi awe na umiliki wa ardhi zoezi litaendelea katika mitaa ambapo mitaa 10 ya kwanza zoezi hilo litafanyika kuanzia jumatatu na mitaa hiyo ni Kibamba, Golani, Mpiji Magoe, Kibangu, Makabe, Tegeta A, Malamba Mawili, Luis, Hondogo na Mji mpya.

“Na mitaa hiyo kumi ni kwaajili ya utambuzi, upangaji, upimaji na umilikishaji na tumeangalia wananchi walio katika hatua ya awali tuwakwamue pia, tunafanya hivyo ili zoezi litakapo malizika katika mitaa mahema yawekwe tena kwaajili ya wananchi kujipatia hati miliki” alieleza Komba

Na kwa wananchi wa Mtaa wa Baruti ni lazima tuweke kikao nao ili tuweze kutafuta suluhu la eneo hilo na kwa Mitaa mingine inayobaki huduma itawafikia.

Nae, Mratibu wa zoezi la ardhi clinik Mkoa wa Dar es Salaam Ndg. Mswani Laurent akielezea mafanikio ya zoezi hilo amesema kuwa ka tika utekelezaji wa mradi huo jumla ya maombi ya hati 1,898 yalipokelewa lakini jumla ya hati 1,692 zimetolewa kwa wananchi sawa na asilimia 89.2.

Aliendelea kueleza kuwa kupitia mradi huu, Serikali imefanikiwa kuingiza mapato kupitia ada na tozo kiasi cha shilingi Milioni 367 na hati 552 zimetolewa kwa jinsia ya ME ,Hati 328 kwa jinsia ya kike, hati 93 kwa umiliki wa pamoja yani mke na mume ,hati 17 kwa makampuni, hati 8 kwa Taasisi mbalimbali.

Changamoto mbalimbali za ardhi ambapo jumla ya migogoro 798 ilitakiwa kufikiwa lakini jumla ya changamoto 528 zimepatiwa majibu,105 zinaendelea kufanyiwa kazi na 165 ni changamoto ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi katika vyombo vya sheria.



# WAJAWAZITO KITUO CHA AFYA MBEZI, WAPATIWA ELIMU YA UPUNGUFU WA DAMU.

Na Mwandishi wetu

Manispaa ya Ubungo kupitia Kitengo cha Lishe kimetoa elimu ya kukabiliana na changamoto ya upungufu wa damu kwa wajawazito ndani ya Kituo cha afya cha Mbezi lengo ikiwa ni kuwawezesha kuepukana na madhara yanayosababishwa na upungufu wa damu kwa wajawazito.

Akielezea madhara ya upungufu wa damu Afisa Lishe wa Manispaa hiyo Onesmo Mwaisyungu alieleza kuwa upungufu wa damu kwa wajawazito unapelekea kuzaa watoto wenye uzito pungufu, upungufu wa maumbile yaani kuwa na kichwa kikubwa, mdomo sungura, mgongo wazi na kupelekea vifo kwa watoto hao lakini pia wajawazito hao hupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua.

Onesmo aliendelea kueleza kuwa, kutokana na madhara hayo Manispaa imeamua kuandaa programu ya kutembelea vituo vya kutolea huduma za afya na kufundisha wajawazito namna bora ya kutengeneza juisi za kuongeza damu ikiwemo juice ya beetroot, rozela na tembele.

Aidha, Onesmo alieleza kuwa beetroot ina faida zaidi ya 19 ikiwemo madini chuma, pia inawezesha kutozeeka mapema, inaimarisha ngozi na inapunguza presha ya kupanda na ameeleza kuwa juisi hiyo inashauliwa kunywa glasi mbili tu kwa siku na kwa matokeo mazuri zinapaswa kunywa asubuhi kabla ya kula kitu chochote huku akisisitiza kwa wenye changamoto ya figo hawaruhusiwi kunywa juisi hiyo.

Sambamba na hayo Onesmo alieleza kuwa wakati wa kutengeneza juisi hizo ni vizuri kuchanganya na pasheni au chungwa au limao au apple au zabibu lakini pia kuongeza na karoti kwenye juisi ya beetroot na zisizidi siku mbili tangu siku ya kutengenezwa na kuhifadhiwa kwenye friji kwa ajili ya matumizi.

Nae Afisa lishe Zulfa Mshitiri akielezea dalili za upungufu wa damu kwa wajawazito hao alisema ni uchovu uliopitiliza, kuishiwa nguvu, kuishiwa pumzi, kupauka ngozi, matatizo ya nywele na kucha na kuvimba miguu, mikono na uso.

Zulfa awataka wajawazito hao kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya mara waonapo dalili hizo huku akiwasisitiza kuhudhuria kliniki ya mama wajawazito, kula vyakula vyenye wingi wa madini chuma na vitamini C lakini pia kunywa dawa za virutubishi ili kuwawezesha kuepukana na madhara ya upungufu wa damu.



# MKURUGENZI UBUNGO ATEMBELEA MIRADI YA MAENDELEO

Na Mwandishi wetu


Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Ndugu Elias Ntiruhungwa alifanya ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya miradi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wasichana ya Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa Shule ya Sekondari King'azi.

Katika ziara hiyo Ntiruhungwa aliagiza majengo yote yaliyofikia hatua ya kupauliwa hadi kufikia wiki ijayo yawe yameshapauliwa ili kuyakamilisha majengo na kuanza kutumika.


Tayari MD Ntiruhungwa aliagiza kazi za umaliziaji katika baadhi ya majengo zikamilike haraka kutoka sasa ikiwemo kazi ya kuweka sakafu pamoja na ufungaji wa gata kwa majengo yote ili kurahisisha uvunaji maji lakini pia kupunguza athari za utiritikaji wa maji katika majengo hayo

Aidha, wakandarasi wanaojenga miundombinu mbalimbali katika Shule ya wasichana ya Dar es Salaam wametakiwa kuwepo site muda wote kuendelea kuchapa kazi ili kukamil-kukamilisha miradi yao kwa wakati.

Tayari jumla ya shilingi Milioni 86 za mapato ya ndani zimekwishatengwa kwa ajili ya urekebishaji wa athari mbalimbali zilizojitokeza kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika Mkoa wa Dar es Salaam na kazi hiyo inatarajiwa kuanza haraka kutoka sasa



*Shule Mpya Maalumu ya Sekondari ya sayansi ya wasichana ya Mkoa wa Dar es salaam iitwayo 'Dar es salaam Girls Secondary School' iliyojengwa Manispaa Ubungo*



*Barabara ya njia nane ya kwanza kujengwa Nchini Tanzania ndani ya Wilaya ya Ubungo kuanzia Kimara hadi Kibaha.*

## IJUE MIRADI MBALIMBALI YA MAENDELEO MANISPAA YA UBUNGO



*Shule Mpya ya Sendari Ubungo NHC ya ghorofa inayoendelea kujengwa ndani ya Manispaa ya Ubungo*



*Pichani ni Shule Mpya ya Msingi Tegeta A*



# MKURUGENZI UBUNGO ATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA KIBIASHARA CHA KIMATAIFA

Na Mwandishi wetu

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo Ndg. Elias Ntiruhungwa alitembelea mradi wa kituo cha kibiashara cha Kimataifa kinachojengwa na Kampuni ya EAST AFRICA COMMERCIAL & LOGISTICS CENTER (EACLC) eneo la Ubungo ilipokuwa stendi ya zamani ya mabasi yaendayo Mikoani na Nchi jirani.

Akiongea wakati anakagua mradi huo Ntiruhungwa alieleza kuwa ujenzi wa Kituo hicho utagharimu Dola za Kimarekani Milioni 118 sawa na Shilingi Bilioni 294 za kitanzania na kitakuwa ni kituo kikubwa na cha kisasa Afrika Mashariki.

Ntiruhungwa aliendelea kueleza kuwa mradi huo utakuwa na jumla ya fremu za ukubwa tofauti tofauti zaidi 2000 na utazalisha ajira za moja kwa moja zaidi ya 15,000 na zisizo za moja kwa moja zaidi ya 50,000 lakini pia utaiwezesha Serikali kuongeza mapato yake.

Sambamba na hayo Ntiruhungwa atoa wito kwa jamii hususani wafanyabiashara kuitumia fursa ya uwepo wa Kituo hicho muhimu kwao na kuwahi kupata fremu za biashara zao ambapo wafanyabiashara wakubwa na wadogo watapata fursa ya kufanya biashara ndani ya kituo hicho.

“Eneo linapojengwa kituo hiki ni eneo rafiki kwa wafanyabiashara kwani linafikika kiurahisi kutokana na uwepo wa miundombinu rafiki ya usafiri ambayo inamuwezesha mtu kufika kwa urahisi kutoka sehemu yeyote ndani na nje ya Mkoa wa Dar es salaam” aliongeza Ntiruhungwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya EACLC Ndg. Catty Wang aliwashukuru Viongozi wa Manispaa ya Ubungo kwa ushirikia no wanaoupata kipindi chote tangu kuanza kwa mradi huo na amesema ujenzi wa mradi huo utakamilika mnamo mwezi Juni 2024 na mara moja biashara zitaanza kufanyika.

Catty aliendelea kueleza kuwa ukamilikaji wa mradi huo utawezesha kukua kwa biashara ndogo ndogo na kupanua biashara hizo ndani ya soko kubwa la Afrika kwani watanzania watapata fursa ya kuagiza na kuuza bidhaa nje ya Tanzania.

Ikumbukwe kuwa Manispaa ya Ubungo iliingia mkataba na Kampuni ya Shanghai Linghang group limited ambaye ni mwekezaji na Kampuni hiyo imeiteua kampuni ya EAST AFRICA COMMERCIAL & LOGISTICS CENTER (EACLC) kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.



# MPANGO WA AWALI WA BAJETI YA LISHE 2024/2025 WAFANYIKA

Na Mwandishi wetu

Manispaa ya Ubungo kupitia idara ya Afya, ustawi wa jamii na lishe imefanya kikao kazi kilicholenga kufanya utekelezaji wa mpango wa awali wa huduma za lishe mtambuka kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Akiongea katika kikao hicho kilichofanyika leo tarehe 24 novemba,2023 Afisa lishe Mkoa Bi. Mwanamvua Zuberi alisisitiza katika uandaaji wa mpango kazi huo ni muhimu kuzingatia vipaumbele ambavyo vitasaidia kuboresha maswala ya lishe na hasa utoaji wa elimu ya lishe mtambuka kwa jamii

Mwanamvua aliendelea kueleza kuwa, ni muhimu mambo yote yanayotakiwa kuzingatiwa katika maswala ya lishe ambayo kwa miaka ya nyuma hayakufanyika kwa sasa yakapewa kipaumbele na marekebisho yote yaliyofanyika katika kuweka maboresho ya mpango kazi ujao yakazingatiwa ili kupata mpango kazi utakaoleta tija kwa jamii.

Akiwasilisha taarifa ya mafanikio ya utekezaji wa lishe kwa mwaka 2022/2023 na robo ya kwanza ya 2023/2024, Afisa lishe wa Manispaa ya Ubungo Bi. Beatrice Mossile amesema kuwa, katika kuhakikisha lishe inakuwa ni swala mtambuka kitengo cha lishe kimefanikiwa kuwafikia wananchi kwa ukaribu zaidi kwa kutoa elimu na pia kuhakikisha ushirikishaji wa viongozi wa Serikali katika siku ya afya na lishe katika ngazi ya mitaa na kata ( SALiKi) umefanyika.

Aliendelea kueleza kuwa, Mafunzo ya matibabu ya utapia mlo yanaendelea kutolewa kwa watoa huduma za afya na pia Utoaji wa elimu ya lishe mashuleni, kuanzisha club za lishe mashuleni ambapo jumla ya shule 213 kati ya 262 zimeanzishwa.

Uhitaji wa vibao vya kupimia urefu, chakula dawa na wadi ya watoto alielezea vinahitajika.

Katika utoaji wa elimu pia wadau mbalimbali wameweza kushirikiana na Manispaa ya Ubungo kwaajili ya utoaji wa elimu ya lishe mashuleni na kwenye jamii, Pia kusaidia watoto waliokutwa na udumavu na Wadau hao ni pamoja na MDH, NCT, TANCO na Jiephaego.

Aidha, Mikakati mbalimbali imewekwa katika mpango wa awali wa huduma mtambuka za lishe kutoka idara na vitengo ikiwemo Idara ya Afya, ustawi wa jamii na lishe, vituo vya huduma za afya, idara za kilimo, uvuvi na mifugo, elimu msingi na sekondari, maendeleo ya jamii, TASAF na Mipango na uchumi



# SOKO LA SIMU 2000 LABORESHWA

Na Mwandishi wetu

“Naipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitahadi zinazofanyika za uboreshaji wa masoko ikiwemo soko la SIMU 2000 kitendo ambacho kinapelekea wafanyabiashara waliotelekeza vibanda vyao ndani ya soko hilo na kwenda kupanga kwenye maeneo yasiyo rasmi kuanza kurudi sokoni”


Kauli hiyo ilitolewa na Ndg. Charles Goodluck mfanyabiashara wa soko hilo wakati alipotembelewa na waandishi wa habari kwa ajili ya kupata maoni ya wafanyabiashara baada ya maboresho yanayoendelea kwenye soko hilo.

Hapo awali soko hilo halikuwa na mazingira rafiki kwa wafanyabiashara hususani kipindi cha mvua lakini vibanda vya awali havikuwa rafiki kwao, kitendo kilichopelekea wafanyabiashara wengi kuondoka kwenye soko hilo na kwenda kufanya biashara kwenye maeneo yasiy rasmi ikiwemo maeneo ya barabarani.

Charles ameendelea kuipongeza Manispaa ya Ubungo kwa ushirikishwaji wa wafanyabiashara juu ya namna bora ya kuboresha soko hilo kwa kuzingatia mahitaji yao ambapo vibanda vilivyojengwa vinamuwezesha mteja kufika kwenye kila kibanda kutokana na jinsi vilivyojengwa kitendo ambacho kinapelekea mzu

Nae Ndg. Zainab Hassan mfanyabiashara wa soko hilo alisema uboreshaji wa soko hilo pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara -

.......Inaendelea ukurasa wa 10



*Vibanda vya wajasiriamali soko la Sim 2000 vikiwa vinaendelea kujengwa*

lakini pia utaiwezesha Manispaa kuongeza mapato yake kwani sasa kila siku tunashuhudia ongezeko la wafanyabiashara wakihitaji kupata vibanda vya kufanya biashara zao.

“Sisi kama wafanyabiashara kwa maboresho haya tupo radhi tena kwa hiari kulipa ushuru na kodi mbalimbali za Manispaa kwani tunaona matunda yake” alisema Zainab.

Kwa upande wake Ndg. Geofrey Mbwama Afisa Mfawidhi sehemu ya Biashara na Masoko Manispaa ya Ubungo amesema katika kutekeleza sera na maagizo ya Mhe. Rais wa awamu ya sita ya kuhakikisha masoko yanaboreshwa, Manispaa ya Ubungo inatekeleza kwa vitendo kwa kufanya uboreshaji wa masoko kwa kutumia fedha za mapato yake ya ndani na Serikali kuu.

Geofrey ameendelea kueleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Manispaa ya Ubungo imeweza kutenga zaidi ya Bilioni 2 Fedha za mapato yake ya ndani kwa ajili ya uboreshaji wa masoko ikiwemo soko la Mabibo, soko la SIMU 2000, soko la Manzese na soko la Mbezi Shule kwa lengo la kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara.

Akielezea ujenzi wa vibanda vya Soko la SIMU 2000 Geofrey ameeleza kuwa Manispaa ya Ubungo kwa kutumia fedha za mapato yake ya ndani kwa awamu ya kwanza ilitenga kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya uboreshaji wa vibanda vya soko hilo na jumla ya vibanda 170 vimejengwa na kwa awamu ya pili kiasi cha shilingi milioni 39 kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa vibanda 80 vya wafanyabiashara ambapo ujenzi upo asilimia 30 na utakamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Akiongelea lengo la maboresho ya soko hilo Geofrey ameeleza kuboreshwa kwa soko hilo ni kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo kuinua vipato vyao sambamba na kuongezeka kwa mzunguko wa biashara, kuwaweka wafanyabiashara pamoja kutokana na aina ya biashara zao na kuongeza mapato ya Manispaa kutokana na ushuru utakaotozwa kwenye vibanda hivyo.

Soko la SIMU - 2000 ni miongoni mwa masoko 13 yanayomilikiwa na Manispaa ya Ubungo ambalo lilianzishwa mwaka 2014 likiwa limejengwa vibanda 312 na baadae wafanyabiashara walihamishwa kutoka kwenye maeneo mbalimbali waliyokuwa wakifanyia biashara ambayo hayakuwa rasmi na kuhamishiwa sokoni hapo lakini waliteleza vibanda vyao kutokana na hali iliyokuwa hapo awali.



# UBUNGO YAJIFUNZA JAMBO ARUSHA JIJI

Na Mwandishi wetu

Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Ubungo wakiongozana na wataalamu wamefanya ziara ya mafunzo katika Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyolenga kujifunza namna bora ya utunzaji wa Mazingira na ukusanyaji wa mapato.

Jiji hilo ambalo limefanikiwa katika ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali, chanzo cha ushuru wa huduma kinachobeba asilimia 35 ya bajeti nzima ya ya Jiji kinafanya vizuri zaidi huku wakieleza siri ya mafanikio hayo kuwa yametokana na kushirikisha taasisi zingine ikiwemo TRA, TARA na TANROADS katika kukusanya ushuru huo.

Akisoma taarifa ya mapato ya ndani ya Jiji hilo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mhasibu msaidizi ndugu Mohamed Koya amesema kuwa manispaa hiyo imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 48.9 kutoka katika vyanzo 32 ikiwemo ushuru wa huduma ambapo kupitia chanzo hicho pekee jumla ya shilingi bilioni 17.5 zinatarajiwa kukusanywa

Vyanzo vingine vinavyofanya vizuri ni pamoja na uuzaji wa viwanja, leseni za biashara, ushuru wa mabango ambapo katika kuhakikisha wanakusanya kwa asilimia 100 mikakati mbalimbali ikiwemo ushirikiano kati ya wataalam na waheshimiwa madiwani katika ukusanyaji, usimamiaji na ufuatiliaji wa mapato kuwa ndilo jambo linalowapa mafanikio makubwa katika ukusanyaji.

Wakiwa kwenya ziara hiyo wana-Ubungo wamejifunza juu ya Matumizi ya mifumo rafiki ya TEHAMA isiyozalisha madeni ambapo baada ya kuoata maelezo ya kina wameamua kutumia wataalamu wa fedha katika Jiji hilo kuwapa mafunzo zaidi ili kutatua changamoto ya wadaiwa sugu na kuchelewa malipo kwa baadhi ya watoa huduma.

Kwa upande wake kaimu Naibu Meya Wa Jiji la Arusha Mhe.Isaya Doita amesema kuwa siri kubwa ya mafanikio ya Halmashauri hiyo katika maeneo mbalimbali ni kushirikiano mzuri uliopo kati waheshimiwa Madiwani na Menejimenti katika kutekekeza shughuli za maendeleo.

Akitoa shukrani katika ziara hiyo Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ubungo Mhe. Jaffary Juma Nyaigesha amesema, pamoja na kupata uzoefu katika ukusanyaji wa mapato, lakini pia wamejifunza namna ya uendeshaji wa dampo ambalo kwa kiasi kikubwa limesaidia kuweka Jiji hilo safi, “tumejifunza na itatusaidia kuendesha dampo letu ambalo tunatarajia kulijenga ili kuimarisha usafi.



# WATENDAJI KATA UBUNGO WATEMBELEA MANISPAA YA MOSHI

Na Mwandishi wetu

Watendaji wa Kata wa Manispaa ya Ubungo wakiongozana na Maafisa Tarafa wa Manispaa hiyo akiwemo Afisa Tarafa wa tarafa ya Kibamba Beatrice Mbawala pamoja na Agnes Kyando Afisa Tarafa wa tarafa ya Magomeni pamoja na Mkuu wa Idara ya Mazingira na Maliasili leo tarehe 21/12/2023 wameitembelea Manispaa ya Moshi kwa lengo la kujifunza masuala ya usimamizi wa usafi wa mazingira.

Akiongea Mkuu wa Kitengo cha mazingira na usafishaji Manispaa ya Moshi Viane Komba amesema Manispaa hiyo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa juu ya usafi wa mazingira kutokana na uwekaji wa mikakati madhubuti iliyowekwa na kusimamiwa na Manispaa hiyo juu ya usimamizi wa usafi wa mazingira

Akiongelea mikakati hiyo Viane amesema Manispaa hiyo imewekavikundi maalumu kwenye Kata zote 21 za Manispaa hiyo ambavyo vimepewa jukumu la kusimamia sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya Manispaa Moshi ya mwaka 2006 iliyofanyiwa marekebisho mwaka mwaka 2017 sambamba na sheria ya mazingira no 20 ya mwaka 2004, sheria ya afya ya jamii no 1 ya mwaka 2009.

Viane ameendelea kueleza kwa mujibu wa sheria ndogo za Manispaa hiyo vikundi hivyo vimepewa nguvu ya kutoza faini ya papo kwa papo isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini kwa wachafuzi wa mazingira na asilimia 50 ya faini inayotozwa hubaki kwa kikundi husika kama malipo kwa wanakikundi.

Aidha, Viane amesema Manispaa hiyo mbali na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa juu ya usimamizi wa usafi wa mazingira pia imefanikiwa kwenye masuala mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa mbolea kwa kutumia taka na hivyo kupunguza taka zinazotupwa dampo na kuongeza mapato ya Manispaa, uwepo wa dampo la kisasa kwa ajili ya kutupa taka na ugatuaji wa shuhuli za usafi wa mazingira katika ngazi ya Kata.

Nae Afisa Mtendaji Kata wa Bondeni Manispaa ya Moshi Philipina Philipo Tenga amesema ngazi ya Kata inajukumu la kuratibu kwa ukaribu shughuli za usafi wa mazingira, kukusanya mapato yatokanayo na ada za taka pamoja na kusimamia matumizi ya Fedha hizo ngazi ya Kata, kuchangia asilimia 3 au 5 ya mapato ya Ada ya taka kwa ajili ya matengenezo ya magari ya kuzoa taka ngumu pamoja na usimamizi wa sheria ndogo kwenye maeneo ya Kata.

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

# HALIUZWI

# JARIDA MTANDAO LA ROBO YA PILI 2023/2024



# UBUNGO FAHARI YETU yetu


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

**MHARIRI: JOINA JIMMY NZALI**

**WAANDAAJI;**

**MARTHA JULIUS**

**TWAGILE SANGA**


Tufuatilie kupitia mitandao ya kijamii ya; ubungomanispaa

Jarida hili linapatikana kwenye tovuti ya Manispaa ya www.ubungomc.go.tz